53	310900002795	Mapambano John Joseph	198,400.00	Duplicate Transaction
54		Shafii Mungu	13,450,000.00	Duplicate Transaction
<b>JUMLA NDOGO</b>			<b>203,636,115.70</b>	
<b>JUMLA KUU</b>			<b>253,718,268.50</b>	



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA CHEMBA



*Unapojibutafadhalitaja;*

**Kumb. Na. CDC/E.10/8 VOLI/142**

**30/01/2025**

Mwenyekiti,  
Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango  
S. L. P 830,  
**CHEMBA.**

**YAH: KUENZISHA MFUKO WA MAENDELEO YA ELIMU NGAZI YA  
HALMASHAURI.**

Husika na mada tajwa hapo juu.

Naomba kuwasilisha taarifa ya uanzishaji wa mfuko wa Elimu ngazi ya Halmashauri.

Kikao cha wataalam wa Elimu na Viongozi ngazi ya Mkoa na Halmashauri kilichofanyika tarehe 05-08 Disemba, 2023 katika Ukumbi wa Chuo cha Ualimu Kondo, moja ya Maazimio yalikuwa Kila Halmashauri na Mkoa kuwa na Mfuko wa Elimu. Kamati ya wataalam wa Halmashauri imejadili na kupendekeza kutengwa kiasi cha shilingi Milioni Arobaini (40,000,000/=) kutoka mapato ya ndani kwa mwaka 2025/2026. Mapendekezo ya matumizi ya fedha hizo ni kama ifuatavyo;-

- uendeshaji wa upimaji wa mitihani ya ndani,
- Ufuatiliaji wa taaluma shuleni,
- kusaidia vifaa, sare na madafdari kwa Watoto wanaotoka mazingira magumu,
- Chakula shuleni.

Hivyo, tunalileta kwenye kikao cha Kamati ya Elimu Afya na Maji ili liweze kupata baraka za uanzishwaji wake.

Nawasilisha.

Siwema H. Jumaa  
**Mkurugenzi Mtendaji (W)**  
**CHEMBA**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



**HALMASHAURI YA WILAYA CHEMBA**

Kumb. Na. CDC/SEC.GEN /VOL.II/113

21/01 /2025

Mwenyekiti  
Kamati fedha,uongozi na mipango  
S. L. P. 830,  
**CHEMBA.**

**YAH: OMBI LA TSH 78,035,770 KWA AJILI YA KUMALIZIA UJENZI WA SHULE  
YA SEKONDARI CHURUKU.**

Husika na somo tajwa hapo juu.

2. Halmashauri ya wilaya ya chemba kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilipokea fedha Tsh. 470,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya Kata ya churuku, miundombinu haikukamilika, Halmashauri iliongezwa Tsh.43,043,000.00 kutoka mapato yake ya ndani ili kuweza kukamilisha vyumba 04 vya madarasa, vyoo vya wanafunzi na kununua madawati 160 na hivyo kuwezesha shule kusajiliwa na kudahili wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 2023. Shule ilikamilika baadhi ya majengo na kuweza kusajiliwa kwa namba S.6117 ya tarehe 23/12/2022 na ilipokea wanafunzi 100. Majengo mengine hayajakamilika hivyo naomba kiasi tajwa ili kiweze kukamilisha shughuli zilizopangwa kufanyika.

Pamoja na barua hii naambatisha BOQ yenye ufafanuzi wa utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kufanyika.

4. Naomba kuwasilisha.

Siwema Jumaa

**MKURUGENZI MTENDAJI  
CHEMBA**

3:



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA CHEMBA**



**Mh. Mwenyekiti**  
**Kamati ya Fedha Uongozi na Mipango.**

**YAH: TAARIFA YA ZOEZI LA CHANJO YA MIFUGO KITAIFA MWEZI JAN 2025**

2. Tarehe 18/12/2024 Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mh. Ashantu K. Kijaji alizindua rasmi zoezi la Uhamasishaji wa Kampeni ya Chanjo ya Mifugo Kitaifa katika hafla maalumu iliyofanyika jijini Dodoma.
3. Chanjo zitakazoanza kutolewa ni CBPP kwa Ng'ombe, PPR kwa Mbuzi na Kondoo na ND kwa Kuku.
4. Aidha chanjo hii itakuwa na ruzuku ya serikali ambapo serikali itagharamia kununua Chanjo, kuwalipa wataalamu, mafuta pamoja na vitendea kazi.
5. Gharama za Chanjo kwa Ng'ombe itakuwa ni Tsh. 500/=, Mbuzi na Kondoo Tsh. 300/= na Kuku ni BURE.
4. kuhusu uukusanyaji wa fedha, kwa mujibu wa muongozo wa utoaji wa chanjo wa Serikaali imeelekeza kila Halmashauri Kufungua akaunti/mfuko maalum (LDF) itakayotumika kukusanyia mapato haya. (kurasa ya Muongozo imeambatishwa)
5. Hatua za maandalizi ya kuanza zoezi zimefikia zaidi ya 90% kilichobaki kwa sasa ni kupokea chanjo na vifaa vya kuchanjia pamoja na maelekezo rasmi kutoka OR-TAMISEMI ya Kufungua akaunti. (Ukurasa wa mwongozo wa utoaji chanjo kitaifa wa mwaka 2024/2025 umeambatishwa)

**3:**

Naomba kuwasilisha.

Kamili F. Makiya  
Kny. Mkurugenzi Mtendaji (H/W)  
Chemba



## **5.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KABLA YA KUTOA CHANJO**

### **5.1 Magonjwa ya kipaumbele yanayohusika na Mwongozo huu**

Kwa kuzingatia athari za magonjwa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP), Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (PPR) pamoja na mdondo wa kuku chanjo dhidi ya magonjwa haya zitatolewa kwa njia ya ruzuku.

### **5.2 Ushirikishwaji wa wadau katika maandalizi na utekelezaji wa utoaji wa chanjo**

Wadau wa utoaji na upokeaji wa huduma ya chanjo wanahitaji kushirikishwa katika maandalizi ili kuwa na uelewa wa pamoja wa umuhimu na kila kinachotegemewa kutokea kutokana na zoezi zima la chanjo. Wafugaji kupitia vyama vya Wafugaji wanahitaji kufahamishwa juu ya malengo ya zoezi husika, kiwango kinachotegemewa kufikiwa, chanjo inayotumika, gharama za kuchanja mnyama na kiasi wanachopashwa kulipia na namna ya kulipia.

### **5.3 Bei Elekezi ya chanjo za magonjwa ya kipaumbele**

Kufuatia Serikali kuweka ruzuku katika kampeni ya kitaifa ya utoaji wa chanjo gharama za chanjo kwa kila mnyama itakuwa kama ilivyo ainishwa kwenye jedwari lifuatalo:

<b>S/N</b>	<b>Ugonjwa</b>	<b>Chanjo</b>	<b>Gharama baada ya ruzuku ya Serikali</b>
1	Mapafu ya Ng'ombe	CBPP	500
2	Sotoka ya Mbuzi na Kondoo	PPR	300
3	Mdondo wa kuku	ND	3Bure

### **5.4 Ukusanyaji na matumizi ya fedha**

Makusanyo ya fedha ya kampeni ya chanjo kitaifa yatakusanywa kwa kutumia POS za mamalaka za serikali za mitaa kwa kutumia mfumo wa ukusanyaji fedha wa TAUS. Fedha zote zitakusanywa katika mfuko maalumu wa maendeleo ya mifugo (LDF) katika kila halmashauri.

Fedha hizi zitatumika kwaajili ya shughuli za chanjo na uchanjaji, udhibiti wa magonjwa na shughuli nyingine za maendeleo ya mifugo.

Mfuko huu utakuwa ukikaguliwa mara kwa mara kwa taratibu za kawaida za ukaguzi wa fedha za serikali katika mamlaka za serikali za mitaa.

## **6.0 SERA, SHERIA NA MIONGOZO INAYOSIMAMIA UTOAJI WA CHANJO ZA WANYAMA**

Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Mifugo ya Mwaka 2006; Sera ya Ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binfasi ya 2009 (National Public-Private Partnership, 2009), Waraka wa Rais Namba 1 wa Mwaka 2002; Hotuba ya Rais ya mwezi Novemba 2020 wakati anazindua Bunge la 12 na Ilani ya CCM 2020-2025 zimetoa mwelekeo kwa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika kutoa huduma za afya ya mifugo ikiwemo utoaji wa chanjo. Pia, utoaji wa huduma ya chanjo kwa kutumia Sekta ya Umma na Sekta Binafsi unasimamiwa na Sheria Na. 17 ya Magonjwa ya Wanyama (The Animal Disease Act) ya Mwaka 2003, na Sheria Na. 16 ya Veterinari (Veterinary Act) ya Mwaka 2003 ambazo kwa pamoja zinasimamia udhibiti wa magonjwa na watoa huduma za mifugo nchini. Pia, Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na 19 ya mwaka 2008 na Marekebisho yake ya Mwaka 2010, inasimamia haki za na ustawi wa wanyama, ikiwemo kukingwa dhidi ya magonjwa vilevile ina mchango wake katika mifumo ya utoaji huduma ya afya ya wanyama. Aidha, Kanuni za Chanjo na Uchanjaji za Mwaka 2020 zinazosimamia chanjo na uchanjaji zinatambua na kuainisha majukumu na mipaka ya wataalamu wa Sekta Binafsi na Sekta Umma na wadau wengine wa pemebejeo, wafugaji katika utoaji na ushiriki kwenye zoezi la chanjo. Hivyo, kwa kuzingatia Sera za kitaifa, Sheria na Kanuni tajwa hapo juu; na maelekezo

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**



**OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA**  
*(Barua zote zielekezwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)*



29/01/2025

Mwenyekiti,  
Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango,  
S. L. P 830,  
**CHEMBA.**

**YAH: KUWASILISHA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA IDARA YA  
UTAWALA NA USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU KWA KIPINDI CHA ROBO YA  
PILI OKTOBA HADI DESEMBA 2024**

Somo hapo juu lahusika.

2. Naomba kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali watu kwa kipindi cha Oktoba hadi Disemba 2024.
3. Pamoja na barua hii naambatisha taarifa hiyo ya utekelezaji wa shughuli hizo.

Naomba kuwasilisha.

Hilary H. Mniachi  
Kny: Mkurugenzi Mtendaji  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA.**

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA IDARA YA UTAWALA NA  
USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU KATIKA KIPINDI CHA ROBO YA PILI  
KUANZIA OKTOBA 2024 HADI DESEMBA 2024**

**1.0 UTANGULIZI.**

Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali watu ina majukumu ya kusimamia masuala ya kiutawala na rasilimali watu. Kazi za Idara hii ni kuratibu vikao vya ngazi ya Halmashauri, Kata na Vijiji, kushughulikia maslahi mbalimbali ya watumishi, kusimamia nidhamu za watumishi mahali pa kazi, kuhakikisha idadi ya watumishi waliopo inaendana na mahitaji ya Ofisi na shughuli nyingine za kiutawala.

**2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA OKTOBA 2024 HADI DESEMBA 2024**

<b>N A</b>	<b>KAZI ZILIZOPANGWA</b>	<b>UTEKELEZAJI</b>
1	Kuratibu na kufanya vikao vya Menejimenti, vikao vya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango na vikao vya kamati nyingine vya mwezi Oktoba 2024 hadi Desemba 2024	Vikao vinaendelea kufanyika kwa mujibu waratiba iliyopo.
2	Kuhakikisha malipo ya mishahara ya Watumishi 1727 wa Halmashauri yameandaliwa na kulipwa katika kipindi chote cha miezi mitatu cha mwezi Oktoba 2024 hadi Desemba 2024	Idara imeandaa mishahara ya miezi mitatu ya Watumishi wote wa Halmashauri yenye thamani ya <b>Tsh. 4,956,239,176.00</b> kwa mchanganuo ufuatao. <ul style="list-style-type: none"> <li>• Mwezi Oktoba , Sh. 1,648,392,392.00</li> <li>• Mwezi Novemba Sh 1,646,455,392.00</li> <li>• Mwezi Desemba, Sh. 1,661,391,392.00</li> </ul>
3	Kushughulikia fomu za mafao ya watumishi wastaafu, waliojifungua pamoja na mirathi na mafao mengine ya watumishi.	Fomu (07) za mafao za watumishi wastaafu, waliojifungua pamoja na mirathi kutoka Idara ya Elimu Msingi, Sekondari, Utawala na Afya zimewasilishwa kwenye Ofisi za Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) kupitia mfumo wa PSSSF member portal kwa ajili ya kushughulikia zoezi la malipo kwa wanufaika.

4	<p>Kuhakikisha kwamba usalama wa Ofisi, vitendea kazi, na nyaraka za Serikali umeimarishwa na kudhibitiwa, kwa kuratibu shughuli za ulinzi wa Ofisi ya Halmashauri, na maeneo mengine yanayolindwa na walinzi wanaolipwa na Halmashauri</p>	<p>Usalama wa Ofisi, vitendea kazi na nyaraka za Serikali umeimarishwa kwa kusimamia walinzi ambao wanalinda kwa sasa.</p>
5	<p>Kufanya ufuatiliaji wa vikao na mikutano ngazi za Kata na Vijiji na kukagua utekelezaji washughuli za Serikali pamoja na kuhakikisha vikao/mikutano yote ya kisheria inafanyika kwenye kata 26 na vijiji 112</p>	<p>Idara imeendelea kuwakumbusha Watendaji wa Kata na Vijiji kufanya Mikutano mikuu kwa kuzingatia ratiba ya vikao hivyo na kuisitiza kuweka Agenda za kudumu zikiwemo kusoma taarifa za mapato na matumizi ili kuimarisha utawala bora na uwajibikaji, taarifa za ulinzi na usalama kusimamia shughuli za maendeleo na kujadili masuala ya jinsia na Ukimwi pamoja na lishe. Vijiji 98 vimefanya Mikutano mikuu ya vijiji na kusoma taarifa ya mapato na matumizi.</p>
6	<p>Kuhakikisha Shughuli za Mfumo wa Mishahara wa Watumishi wa Serikali (e-Watumishi) zinafanyika kwa wakati kwa kila mwezi mfano: kufuta watumishi waliofariki, kustaafu kazi kwa hiari n.k</p>	<p>Watumishi watano (05) wameondolewa kwenye Mfumo wa Mishahara wa Halmashauri ya Chemba kwa sababu ya kustaafu kazi kwa lazima na hiari na kifo.</p>

7	Kuandaa madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi na kuingiza kwenye mfumo wa malipo mishahara (HCMIS)	Ofisi imefanya zoezi la kuingiza taarifa kumi na mbili (12) za watumishi wenye madai ya malimbikizo ya mishahara kwenye mfumo wa taarifa za kiutumishi na mishahara (HCMIS) kwa ajili ya kupata idhini toka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kisha kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu Hazina kwa ajili ya malipo. katika kipindi cha robo ya pili watumishi wawili (02) wamelipwa malimbikizo ya mishahara yenye kiasi cha <b>4,028,000.00/=</b>
8	Kuidhinisha mikopo ya Watumishi	Idara imehakikisha kwa kipindi cha mwezi Oktoba hadi Desemba 2024 imepitisha makato ya watumishi kwenye mfumo wa HCMIS kupitia Bank/kampuni ya NMB, CRDB, Bayport, Letshego, Platinum Ltd, Maboto Enterprises, ABC, Tanzania Commercial Bank, Equity Bank, Mwalimu Commercial Bank, Fanikiwa ambapo kwa sasa watumishi wote ni lazima waombe mkopo kupitia mfumo wa ESS.
9	Kuandaa taarifa ya Tume ya Utumishi wa Umma (TUU)	Kwa kipindi cha robo ya pili Idara imeandaa taarifa ya Tume ya Utumishi wa Umma na kuzituma kwa Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma kwa ajili ya hatua ya ufuatiliaji na ukaguzi wa uendeshaji wa shughuli za kiutumishi.
10	Kushughulikia taratibu za uhamisho ndani na nje ya Halmashauri.	Kwa kipindi cha mwezi Oktoba hadi Desemba 2024 Idara imehakikisha Mishahara ya watumishi ishirini na tisa (29) imehamishwa kwenda kwenye Halmashauri/ Taasisi walizohamia kwa kuwasilisha orodha ya majina hayo kwenye mamlaka za uhamisho kwakuwa ndio zenye idhini ya kufanya uhamisho wa watumishi kwenye mfumo. Kiambata 1

11	Kuratibu zoezi la kuwapokea watumishi wa ajira mpya waliopangiwa kazi na mamlaka mbalimbali ikiwemo Ofisi ya Rais Tamisemi na Katibu Mkuu utumishi na kuingiza taarifa zao kwenye mfumo wa malipo ya mshahara kwa ajili ya uhidhinishwaji wa kupata cheki namba	Kwa kipindi cha mwezi Oktoba hadi Desemba 2024 Halmashauri imepokea na kuajiri watumishi arobaini na nane (48) waliopangiwa kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Chemba kutoka Ofisi ya Rais Sekretarieti ya ajira katika Utumishi wa Umma kwa utekelezaji wa vibali vya ajira Mpya kwa watumishi .
----	---	---

### 3.0 CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI NA UTATUZI

NA	CHANGAMOTO	UTATUZI WA CHANGAMOTO
1	Upungufu mkubwa wa Watumishi kwa kada mbalimbali za Halmashauri hususani, Idara ya Afya, Idara ya Ujenzi na Zimamoto, Idara ya Utumishi na Utawala na Idara ya Fedha na Biashara.	<ul style="list-style-type: none"> <li>i. Kuendelea kuandaa Makadirio ya Ikama na Bajeti ya Mishahara kila mwaka na kuwasilisha Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.</li> <li>ii. Kufanya mawasiliano na Katibu Mkuu (TAMISEMI) na Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma kuhusu kupangiwa watumishi wengine ili kupunguza uhaba wa watumishi.</li> </ul>
2	Malipo ya stahiki za uhamisho wa watumishi wa ndani na nje ya Halmashauri.	<ul style="list-style-type: none"> <li>i. Kufanya mawasiliano na Ofisi ya Katibu Mkuu Wizara ya Fedha ili iweze kusaidia kulipa madai hayo kwa kuwa Halmashauri haina mapato ya kutosheleza.</li> </ul>

**KIAMBATA NAMBA 1: ORODHA YA WATUMISHI WALIOHAMA.**

<b>NA</b>	<b>JINA LA MTUMISHI</b>	<b>IDARA/KITENGO</b>	<b>TAASISI ALIYOHAMIA</b>
1	Jeneroza Mwita Mtete	Elimu Msingi	Halmashauri ya Jiji la Dodoma
2	Emmanuel Yohana Solomoni	Elimu Msingi	Halmashauri ya Wilaya ya Muleba
3	Yohana Lingson Mbeyanje	Elimu Sekondari	Halmashauri ya Jiji la Mbeya
4	Mariam Nyanda Elisha	Elimu Sekondari	Halmashauri ya Manispaa ya Singida
5	Dawia Ally Yusufu	Elimu Msingi	Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli
6	Mohamed Hemedi Ngotwike	Elimu Msingi	Halmashauri ya Wilaya ya Ileje
7	Husna Shukuru Mvungi	Elimu Msingi	Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo
8	Thabit Salum Litatiro	Elimu Sekondari	Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro
9	Shadia Twahili Kato	Utawala	Chuo Kikuu cha Dodoma
10	Hadija Khamisi Tajiri	Afya	Halmashauri ya Jiji la Mwanza
11	Elia Bukuku Ambukege	Afya	Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe
12	Naomi Julius Mbwanje	Elimu Msingi	Halmashauri ya Wilaya ya Ileje
13	Imani Vicenti Mauya	Afya	Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo
14	Vicent Zebedayo Mwalongo	Elimu Msingi	Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo
15	Elias Thomas Mayunga	Elimu Sekondari	Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe
16	Ansila Isdory Mbiro	Elimu Msingi	Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo
17	Rehema Daruweshi Abdallah	Afya	Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga



18	Aloycia Anna Komba	Elimu Msingi	Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo
19	Noel Mussa Dohodoho	Elimu Msingi	Halmashauri ya Jiji la Dodoma
20	Stella Hamisi Mrope	Afya	Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro
21	Josephine Anthony Kalikawe	Elimu Msingi	Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro
22	Neema Gabriel Ghamunga	Elimu Msingi	Halmashauri ya Wilaya ya Babati
23	Jacqueline John Lihame	Elimu Msingi	Halmashauri ya Manispaa ya Temeke
24	Langson David Nkwamu	Elimu Msingi	Halmashauri ya Wilaya ya Arusha
25	Yuster L.Chamanga	Elimu Msingi	Halmashauri ya Manispaa ya Ilala
26	Chacha Daniel Joseph	Elimu Msingi	Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto
27	Bahati Bakari Rashidi	Elimu Sekondari	Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro
28	Beatrice Emmanuel Mkumbwa	Elimu Sekondari	Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba
29	January Nilasco Nyongole	Elimu Msingi	Halmashauri ya Wilaya ya Madaba

#### KIAMBATA NAMBA 2: ORODHA YA WATUMISHI WALIOHAMIA

NA	JINA LA MTUMISHI	IDARA/KITENGO	TAASISI ALIYOTOKA
1	James Dalasia James	Fedha na Uhasibu	Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA CHEMBA



MHESHIMIWA MWENYEKITI,  
KAMATI YA MIPANGO, FEDHA NA UONGOZI

29 Januari, 2025

H/W CHEMBA.

**TAARIFA YA ROBO YA PILI YA DIVISHENI YA VIWANDA, BIASHARA NA  
UWEKEZAJI YA MWAKA 2024/2025**

Mh; Mwenyekiti naomba kuwasilisha taarifa ya robo ya pili ya Divisheni ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Katika kipindi hicho cha robo kwa pili ya mwaka wa fedha 2024/2025 yaani Octoba 01 hadi Disemba 31, Divisheni ilitekeleza shughuli zifuatazo;

1. Divisheni iliendelea kuhamasisha, kutoa elimu na ukusanyaji wa leseni za biashara ambapo kwa kipindi hicho Halmashauri imetoa jumla ya leseni za biashara 115 ambapo shilingi 16,470,500/= zilikusanywa. Mchanganuo wa idadi na aina ya leseni zilizotolewa umeambatishwa katika kiambata A.
2. Divisheni iliendelea kufanya ukaguzi na urasimishaji wa nyumba za kulala wageni kwa mujibu wa sheria na kupelekea ukusanyaji wa shilingi 2,428,500/=.
3. Divisheni iliendelea na zoezi la urasimishaji na utoaji wa leseni za vileo kwa mujibu wa sheria ambapo jumla ya leseni 31 za vileo zilitolewa na shilingi 664,000/= zilikusanywa. Taarifa ya mchanganuo wa leseni za vileo zilizotolewa upo kwenye Kiambatisho A.
4. Divisheni iliendesha zoezi la udhibitisho wa takwimu za mabango ya biashara kwa wafanyabiashara binafsi, mabenki na makampuni ambapo Katika kipindi hicho jumla ya shilingi 9,444,710.5 zilikusanywa kama ushuru wa mabango.

- 5 Kutokana na mwongozo wa serikali wa kuendelea kuwatambua na kurasimisha biashara za wajasiriamali wadogo Divisheni iliendelea na zoezi la kuwasajili wajasiriamali wadogo na machinga kwa kushirikiana na Divisheni ya Maendeleo ya jamii

### **Changamoto za utekelezaji;**

Mh; Mwenyekiti Divisheni ya viwanda,biashara na uwekezaji inakabiliwa na changamoto zifuatazo kiutendaji

1. Baadhi yawafanyabiashara kutokua na elimu ya kutosha juu ya wajibu wao wa kulipa leseni kwa hiyari pindi wanapoanzisha biashara au kuendelea kufanya biashara bila kuhuisha leseni.Pia wafanyabishara wengi kuwa kwenye shughuli za kuandaa mashamba na kilimo hivyo kusababisha kufunga maduka.
2. Baadhi ya makampuni na watu binafsi kutotii takwa la kisheria la kulipa ushuru wa mabango kwa hiari.

### **Mikakati ya kukabiliana na Changamoto.**

1. Divisheni inaendeleza uhamasishaji na utoaji elimu kwa wafanyabishara ili kutimiza wajibu wa kulipa ada ya leseni za biashara,leseni za vileo na tozo mbalimbali ambazo zipo kwa mujibu wa sheria na pia kuendesha biashara kwa kufuata sheria.
2. Divisheni imewaandikia notisi ya kisheria ya madai ya ushuru wa mabango kwa wadaiwa ambapo tayari kampuni na benki 9 zimetumiwa notisi za madai. Halmashauri itawafikisha mahakamani wale ambao hawatalipa ushuru huo kwa hiari.

4,

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kuwasilisha.

Inyasi .I. Priscusi  
Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Viwanda,Biashara  
na Uwekezaji (W) Chemba

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA CHEMBA  
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)



29/01/2025

NDUGU MWENYEKITI,

Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango,

S.L.P 830 – CHEMBA.

**YAH: TAARIFA YA UTENDAJI KAZI WA KITENGO CHA SHERIA KWA KIPINDI  
CHA MWEZI OKTOBA MPAKA MWEZI DISEMBA 2024.**

**Ndugu Mwenyekiti,**

Kwa kipindi cha robo ya pili ya mwaka, kitengo cha huduma za kisheria kimekuwa kikifanya kazi mbalimbali vizuri kwa kushirikiana na Divisheni na vitengo vingine ndani ya Halmashauri ya wilaya ya Chemba.

Ndugu mwenyekiti, taarifa hiyo ina sehemu tatu (3) na jedwali moja mwishoni mwa taarifa hii. Sehemu ya Kwanza ni utangulizi, ya Pili ni shughuli zilizofanyika kwa kipindi cha Oktoba hadi Disemba (robo ya pili ya mwaka 2024/25) na ya Tatu ni shughuli zinazotarajiwa kufanywa na kitengo cha sheria kwa kipindi cha mwezi January hadi Machi 2025. Sehemu ya mwisho ni jedwali linaloonyesha mashauri mbalimbali ambayo halmashauri imeshtaki na kushtakiwa pamoja na hatua ambazo hizo kesi zipo kwa sasa.

Ndugu mwenyekiti,

Naomba kuwasilisha.

4!

.....

Dominic Ruhamvya

Mkuu wa Kitengo cha huduma za Sheria (H/W) Chemba.

## **1.0 UTANGULIZI**

Ndugu Mwenyekiti;

Kwa kipindi cha robo ya pili ya mwaka, kitengo cha huduma za kisheria kimekuwa kikifanya kazi mbalimbali vizuri kwa kushirikiana na Divisheni na vitengo vingine ndani ya Halmashauri ya wilaya ya Chemba.

## **2.0 SHUGHULI ZILIZOFANYIKA KWA KIPINDI CHA OKTOBA HADI DISEMBA (ROBO YA PILI YA MWAKA 2024/25)**

Ndugu mwenyekiti;

Kwa kipindi tajwa hapo juu, kitengo cha sheria kimefanya kazi zifuatazo:-

- i. Kufanya uhakiki (vetting) wa mikataba ya ujenzi wa majengo mbalimbali, kama vile katika Shule ya sekondari Gwandi.
- ii. Kuiwakilisha Halmashauri ya wilaya ya Chemba Mahakamani, katika Mashauri yaliyopo kwenye Jedwali lililoko ukurasa wa mwisho wa taarifa Hii.
- iii. Kutoa ushauri mbalimbali wa kisheria kwa Vitengo/Divisheni za Halmashauri na Menejimenti yake.
- iv. Kupokea kero na migogoro mbalimbali ya kisheria kutoka kwa wananchi wa wilaya ya Chemba na kuzitatua au kutoa miongozo wa jinsi ya kuzitatua.
- v. Kuandaa nyaraka mbalimbali za kisheria zinazoihusu Halmashauri.

## **3.0. SHUGHULI ZINAZOTARAJIWA KUFANYWA NA KITENGO CHA SHERIA KWA KIPINDI CHA MWEZI JANUARY HADI MACHI (ROBO TATU YA MWAKA 2024/2025).**

- a. Kuyatembelea mabaraza matatu (3) ya kata yaliyopo katika Halmashauri hii na kutoa Elimu juu ya uendeshaji wa Mashauri ya Ardhi na Mashauri Mengine ambayo yako chini ya Mamlaka ya Mabaraza ya Kata.
- b. Kuendelea kushughulika na Mashauri ambayo bado hayajafikia hatua ya Hukumu/Uamuzi, Mashauri yaliyopo kwenye Jedwali lililoko ukurasa wa mwisho wa taarifa.
- c. Kuendelea Kutoa Ushauri wa Kisheria kwa Halmashauri na Menejimenti yake.
- d. Kufanya Kazi mbali mbali kama itakavyoelekezwa au Kuagizwa na Mkurugenzi.

**Ndugu Mwenyekiti,**

**JEDWALI LA MASHAURI**

Na	TAARIFA YA KESI	MAELEZO MAFUPI	HATUA
1.	Abdilah Shaban Mriri versus Mohamed Pampay, Chemba District Council and the Attorney General, Land Case No. 8793 of 2024, High Court of Tanzania (Dodoma District Registry), At Dodoma;	Hii ni Kesi ya Ardhi ambayo Mdai anaadai kwamba Mdaiwa Wa Kwanza Bw Mohamed Pampay alipewa Kiwanja na Halmashauri baada ya Upimaji uliofanyika mwaka 2014, kwamba kiwanja hicho alitakiwa apewe yeye.	Tarehe 04/01/2025 Imepangwa kusikilizwa mapingamizi ya Awali
2.	Mumba Juma Mumba v. Chemba District Council and the Attorney General, Land Case No. 9370 of 2024, High Court of Tanzania (Dodoma District Registry), At Dodoma;	Hii ni Kesi ambayo Halmashauri inadaiwa kushindwa kumlipa Mkandarasi Retention Money baada ya Kumaliza kujenga Shule ya Sekondaari ya Msaada mwaka 2018	Tarehe 06/01/2025 Imepangwa Kutolewa uamuzi Mdogo baada ya kusikilizwa mapingamizi ya Awali ya kisheria.
3.	Kidoka Village Officer, Kidoka Village Coucil, the District Commisioner for Chemba District, the Permanent Secretary, President's Office, Regional Administration and Local Government and The Attorney General Versus Petro Chacha	Hii ni kesi ya rufaa kutoka mahakama kuu kwenda mahakama ya rufaa ya Tanzania, na kwa sasa kesi hiyo ipo hatua ya kuskilizwa.	Ipo hatua ya kusikilizwa Tunasubiri Tarehe ya Vikao vya Mahakama ya rufani 4

	and Chambiri Mwita Mniko		
--	-----------------------------	--	--

.....

Dominic Ruhamvya

Mkuu wa Kitengo cha huduma za Sheria (H/W) Chemba.



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA**



Kumb.Na.CDC/E.30/2VOLII/96

**Mhe. Mwenyekiti,**  
Kamati ya fedha uongozi na Mipango,  
S.L.P 830,  
**CHEMBA.**

30/12/2025

**YAH: TAARIFA YA KITENGO CHA UCHAGUZI ROBO YA PILI OKTOBA - DISEMBA  
2024/2025**

**Mhe. Mwenyekiti**

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu.

2. Naomba kuwasilisha taarifa ya shughuli za kitengo cha uchaguzi
3. Taarifa hii inahusisha shughuli za uchaguzi zilizofanyika kwenye robo ya pili ya oktoba-Disemba 2024/2025. Shughuli hizi zimegawanywa kwenye makundi mawili
- A. Mchakato mzima wa uchaguzi wa Viongozi wa Serikali za Mitaa ngazi ya Vijiji na Vitongoji Mwaka 2024 katika Halmashauri ya Wilaya ya Chemba.
  - Maeneo ya Utawala yaliyofanya uchaguzi
  - Uhamasishaji na Utoaji Elimu ya Mpiga Kura
  - Semina kwa Viongozi na Watumishi waliosimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa
  - Uandikishaji wa wapigakura
  - Uteuzi wa wagombea na kampeni za uchaguzi
  - Upigaji kura na Matokeo ya Uchaguzi
  - Ushiriki wa asasi za kiraia
  - Mafanikio na changamoto.
- B. Zoezi la Uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa Rais, wabunge na Madiwani wa mwaka 2025.
  - Mapokezi ya Vifaa kwa ajili ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura
  - Semina kwa Maafisa Waandikishaji Wasaidizi ngazi ya Kata, Waandishi na BVR Kit Operators
  - Kuanza kwa zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kutumia mfumo wa BVR
  - Mafanikio na Changamoto

4!

**Mhe. Mwenyekiti**

Taarifa ya kina imeambatishwa kwenye barua hii. Aidha taarifa husika imezingatia matukio yaliyoainishwa kwenye ratiba ya kuu ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024 pamoja na mfululizo wa matukio wakati wa uboreshaji wa daftari.

**Mhe. Mwenyekiti,**

Naomba kuwasilisha.

Tamko Ngumbuke  
Kny: Mkurugenzi Mtendaji (H/W),  
**CHEMBA.**



# **TAARIFA YA KITENGO CHA UCHAGUZI ROBO YA PILI YA OKTOBA-DISEMBA 2024/2025**

## **1.0. Utangulizi**

Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ni miongoni mwa Halmashauri za Mkoa wa Dodoma zilizoendesha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024. Sambamba na kuendesha uchaguzi wa Serikali za mitaa, Jimbo la Chemba ni miongoni mwa Majimbo kumi (10) yaliyopo katika Mkoa wa Dodoma ambayo yalishiriki katika uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura 2024 ikiwa ni maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025. Shughuli hizi zote zilifanyika katika robo ya pili ya Oktoba-Disemba 2024/2025.

## **SEHEMU A: UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA**

### **2.0. MAANDALIZI, URATIBU NA UENDESHAJI WA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA 2024**

Uchaguzi wa Serikali za mitaa uliendeshwa kwa kuzingatia kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji za Mwaka 2024, (Tangazo la Serikali Na.571 la tarehe 12/07/2024, Mwongozi wa Uchaguzi wa ngazi za Vijiji, Vitongoji na Mitaa na kwa Ratiba ya Matukio ya Uchaguzi. Nafasi zilizogombewa ni mwenyekiti wa kijiji, wajumbe wa Halmashauri ya kijiji na mwenyekiti wa kitongoji. Utekelezaji wa shughuli hizi ulianza rasmi baada ya tangazo la uchaguzi kwa umma la tarehe 15 agosti 2024.

Vyama Vinne (4) vya Siasa viliteua Wagombea kuwania nafasi za Uongozi wa Serikali za Mitaa. Vyama hivyo ni (C.C.M), (CHADEMA), (C.U.F) na NCCR Mageuzi.

#### **2.1. Maeneo ya Utawala yaliyofanya uchaguzi**

Maeneo yaliyoshiriki uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024 ni yale yaliyotangazwa rasmi na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 16/09/2024 ambapo Wilaya ya Chemba ina jimbo 1 la uchaguzi lenye ukubwa wa kilomita za mraba 7653, ina Tarafa nne, kata 26, Vijiji 114 na vitongoji (Vituo) 488 vya kuandikisha orodha ya wapigakura na kupigia kura

#### **2.2. Uhamasishaji na Utoaji Elimu ya Mpiga Kura**

Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ilikuwa na mikakati ya uhamasisha na utoaji wa elimu kwa mpigakura katika hatua zote mhimu za zoezi la uchaguzi kuanzia maandalizi ya uchaguzi, zoezi la uandikishaji, na zoezi la upigaji kura. Mifumo iliyotumika kufanya uhamasishaji na utoaji elimu ya mpigakura ni pamoja na kutumia gari la Matangazo (PAsystem), Whatsapp message, mabonanza, elimu kupitia makundi mbalimbali, pamoja na mfumo wa kawaida wa Matangazo vijijini ikiwemo kupiga debe, Ngoma na matangazo kwenye mbao za Matangazo.

2.3. Semina kwa Viongozi na Watumishi waliosimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa

**Jedwali 3: Mafunzo ya Uchaguzi Yaliyotolewa**

Na.	Aina ya Semina	Washiriki	Waandaaji na Waendeshaji wa Semina
1	Mafunzo kwa wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata na vijiji	Wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata 26 na vijiji 112	Msimamizi wa uchaguzi
2	Mafunzo kwa waandikishaji na waandaaji wa orodha ya wapigakura	Waandikishaji na waandaaji wa orodha ya wapigakura 488	Msimamizi wa uchaguzi
3	Mafunzo kwa kamati ya rufaa	Kamati ya rufaa ya wilaya chini ya katibu tawala wa Wilaya	Msimamizi wa uchaguzi
4	Mafunzo kwa wasimamizi wa vituo na wasimamizi wasaidizi wa vituo	Wasimamizi wa vituo 488, wasimamizi wasaidizi wa vituo 488 na wasimamizi wa ziada 26	Msimamizi wa uchaguzi

3.0. UANDIKISHAJI WA WAPIGA KURA

Uandikishaji na uandaaji wa orodha ya wapigakura ulifanyika kwa siku 10 kuanzia tarehe 11-20/10/2024. Lengo ilikuwa ni kuandikisha na kuandaa orodha ya wapiga kura 175,566 (wanaume 87,354 na wanawake 88,212).

3.1.1. Matokeo ya Uandikishaji Wapiga Kura

Katika zoezi la uandikishaji na uandaaji wa orodha ya wapiga kura, jumla ya wapigakura 194,230 sawa na asilimia 110.8 ya malengo waliandikishwa ambapo Wanaume walikuwa 99,352 sawa na asilimia 113.7 na wanawake walikuwa 94,878 sawa na

4.0. Pingamizi na Rufaa kwa Waliojiandikisha Kupiga Kura

Orodha zilibandikwa tarehe 21/10/2024 na usikilizaji wa mapingamizi ulikuwa kwa siku saba tarehe 21-27/10/2024. Hatukupokea pingamizi lolote juu ya orodha

5.0. Ushiriki wa Vyombo vya Usalama katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa<sup>5</sup>

Vyombo vya usalama vilishiriki katika kulinda na kuhakikisha amani kila eneo katika hatua na michakato yote ya uchaguzi wa Serikali za mitaa 2024 ikiwa ni pamoja na usimamizi shirikishi kwa Mamlaka na vyombo vyote vinavyohusika na shughuli za uchaguzi

6.0. UTEUZI WA WAGOMBEA NA KAMPENI ZA UCHAGUZI

Zoezi la utoaji wa fomu za uteuzi wa wagombea lilianza tarehe 26/10/2024 na lilikamilika tarehe 1/11/2024. uteuzi wa wagombea ulifanyika tarehe 8.11.2024

6.1. Uteuzi wa Wagombea

Nafasi za uongozi zilizogombewa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024 kwa ngazi zote ilikuwa ni nafasi **4** katika mchanganuo ufuatao:

- a) Nafasi za Wenyeviti wa Vijiji zilipaswa kuwa **114**
- b) Nafasi za Wenyeviti wa Vitongoji zilipaswa kuwa **488**
- c) Nafasi za Wajumbe Kundi la Wanawake zilipaswa kuwa **912** na
- d) Nafasi za Wajumbe Kundi Mchanganyiko zilipaswa kuwa **1336**

6.1.1. Utaratibu wa uchukuaji na urejeshaji wa fomu za maombi ya kuteuliwa kugombea nafasi mbalimbali za uongozi waombaji Walioteuliwa Kugombea Nafasi Mbalimbali za Uongozi

Kufuatia uteuzi huo, waombaji 3393 waliteuliwa kugombea nafasi mbalimbali za uongozi. Idadi hii ya wagombea ni sawa na asilimia 95 ya waombaji 3582 waliorejesha fomu. Mchanganuo wa wagombea walioteuliwa kwa kila nafasi ya uongozi ni kama ifuatavyo:

- a) Nafasi za Wenyeviti wa Vijiji waliteuliwa wagombea 151 kutoka Vyama vinne vya CCM, CHADEMA, CUF NA NCCR Mageuzi sawa na asilimia **85** ya waombaji wote **177** waliorejesha fomu.;
- b) Nafasi za Wenyeviti wa Vitongoji waliteuliwa wagombea 572 kutoka Vyama vitatu (3) vya CCM, CHADEMA, CUF sawa na asilimia **91** ya waombaji wote **632** waliorejesha fomu za kugombea nafasi hizo.;
- c) Nafasi za Wajumbe wa Halmashauri za Vijiji kundi la Wanawake waliteuliwa wagombea 1041 sawa na asilimia **97** ya waombaji 1071 waliorejesha fomu za kugombea uongozi kwa nafasi hizo;
- d) Nafasi za Wajumbe wa Halmashauri za Vijiji Kundi Mchanganyiko waliteuliwa wagombea **1629** sawa na asilimia **96** ya waombaji **1702** waliorejesha fomu za kugombea nafasi hizo.

**Jedwali 5: Uwiano wa Idadi ya Waombaji Waliorejesha Fomu na Walioteuliwa Kugombea Nafasi za Uongozi (uenyekiti kijiji na kitongoji) katika vyama**

Chama	Mwenyekiti wa Kijiji		Mwenyekiti wa Kitongoji	
	Walio rejesha Fomu	Walio teuliwa	Walio rejesha Fomu	Walio teuliwa
CCM	114	114	488	488
CHADEMA	40	24	97	53
CUF	21	12	47	31
NCCR Mageuzi	2	1	0	0
<b>Jumla</b>	<b>177</b>	<b>151</b>	<b>632</b>	<b>572</b>

6.1.2. Pingamizi na Rufaa Dhidi ya Uteuzi wa Wagombea

**Jedwali 6: Idadi ya Pingamizi na Rufaa Zilizopokelewa na Zilizoshinda kwa Wilaya**

Halmashauri	Idadi ya Pingamizi		Idadi ya Rufaa	
	Zilizopokelewa	Zilizoshinda	Zilizopokelewa	Zilizoshinda
CHEMBA	56	50	32	18
	<b>56</b>	<b>50</b>	<b>32</b>	<b>18</b>

6.1.3. Wagombea Waliojitoa na Walioondolewa Dhamana na Vyama Vyao

**Jedwali 7: Idadi ya Wagombea Waliojitoa na Vyama Husika**

Chama	Wenyeviti			Wajumbe Halmashauri ya Kijiji	
	Vijiji	Mitaa	Vitongoji	Wanao	Mchanganyiko
CHADEMA	5		5	0	0
CUF	1		0	0	0
<b>Jumla</b>	<b>6</b>		<b>5</b>		

6.2. Ukomo wa Kuwepo Madarakani kwa Viongozi Waliopita.

Viongozi wa serikali ya kijiji waliokuwa madarakani walikoma kuwa kwenye nyadhifa zao na kukabidhi ofisi kwa watendaji tarehe 19/10/2024 na mpaka kufikia tarehe 21/10/2024 viongozi wote walikuwa wamekabidhi ofisi.

6.3. Kampeni za Uchaguzi

Kampeni za uchaguzi zilifanyika kwa muda wa siku saba kuanzia tarehe 20-26/11/2024 na jumla ya vyama vyote vine vilishiriki kampeni hizi

**7.0. UPIGAJI KURA NA MATOKEO YA UCHAGUZI**

Kati ya Wapiga Kura wote waliojiandikisha kwenye maeneo yaliyofanya Uchaguzi, Wapiga Kura wafuatao walijitokeza kupiga Kura siku ya Uchaguzi tarehe 27 Novemba, 2024: -

**Jedwali 8. Wapiga Kura waliojitokeza Kupiga Kura Siku ya Uchaguzi**

Ngazi ya Uongozi	Idadi ya Waliojiandikish	Idadi ya Waliopiga Kura	Asilimia ya Waliopiga Kura
Nafasi ya Mwenyekiti wa Kijiji	194,230	188,015	96.8
Nafasi ya Mwenyekiti wa	194,230	188,015	5: 96.8

7.1. Matokeo ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024

Matokeo ya ujumla kwa viongozi waliochaguliwa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024 ni kama ilivyoainishwa katika jedwali hapo chini:

**Jedwali 9: Idadi ya Viongozi Walioshinda Katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024 kwa Vyama**

<b>Vyama</b>	<b>Mwenyekiti wa Kijiji</b>	<b>Mwenyekiti wa Kitongoji</b>	<b>Wajumbe Kundi la Wanawake</b>	<b>Wajumbe Kundi Mchanganyiko</b>
CCM	111	474	912	1336
CHADEMA	1	9	0	0
CUF	2	5	0	0
NCCR MAGEUZI	0	0	0	0
<b>Jumla</b>	<b>114</b>	<b>488</b>	<b>912</b>	<b>1336</b>

7.2. Ushiriki wa Makundi Maalum (Wanawake na Vijana) katika Uchaguzi

**Jedwali 11. Idadi ya Wanawake na Vijana Walioshinda Nafasi za Uongozi**

<b>Nafasi ya Uongozi</b>	<b>Jumla ya</b>	<b>Wanawake waliochaguliwa</b>	<b>%</b>	<b>Vijana Waliochaguli</b>	<b>%</b>
Mwenyekiti wa Kijiji	114	1	1	39	34
Mwenyekiti wa Kitongoji	488	29	6	194	40
<b>Jumla</b>	<b>602</b>	<b>30</b>	<b>5</b>	<b>233</b>	<b>39</b>

**8.0. USHIRIKI WA TAASISI NA ASASI ZA KIRAIA KATIKA UTOAJI WA ELIMU NA UANGALIZI WA UCHAGUZI**

Asasi za kiraia ni taasisi binafsi zilizopewa kibali na OR-TAMISEMI kuwa waangalizi wa shughuli za uchaguzi pamoja na kutoa elimu ya mpiga kura. Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ilipata Asas moja ya kiraia inayoitwa TANLAP iliyoshiriki katika uangalizi wa michakato yote ya Uchaguzi pamoja na Kutoa elimu kwa mpigakura.

**9.0. MAFANIKIO NA CHANGAMOTO ZA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA WA MWAKA 2024**

5,

- Mafanikio yaliyopatikana ikilinganishwa na chaguzi za nyuma ni kwanza bajeti iliyopangwa kuletwa kwa asilimia 100
  - Shughuli za Uchaguzi kufanyika kwa mujibu wa Ratiba ya matukio ya Uchaguzi.
  - Uchaguzi kufanyika kwa amani na utulivu zaidi
  - Mwamko mkubwa wa wananchi kujitokeza kugombea nafasi za uongozi kuanzia Mwenyekiti wa Kijiji, Kitongoji na Ujumbe wa Halmashauri za Vijiji.
  - Kufanya maandalizi ya vifaa vya uchaguzi kwa wakati
- ✓ Changamoto na namna zilizovyotatuliwa
    - Uchache wa vituo /vitongoji vya kupigia kura ukilinganisha na ongezeko la idadi ya watu
  - ✓ Mapelelezo ya kuboresha chaguzi zingine
    - Serikali iendelee kutoa fedha za kuendesha shughuli za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kama zilizvyotengwa kwenye Bajeti za Halmashauri.

- Elimu ya Mpiga Kura iendelee kutolewa kwa wananchi badala ya kusubiri elimu hiyo kutolewa kipindi cha Uchaguzi pekee.
- Vyama vya siasa vishiriki kikamilifu kwenye shughuli za Uchaguzi ili kuendelea kuimarisha demokrasia ya vyama vingi nchini.

## **10.0. HITIMISHO**

Viongozi waliochaguliwa kwa ngazi zote waliapa na kuanza kutekeleza majukumu yao tarehe 29/11/2024.

## **SEHEMU B: TAARIFA YA ZOEZI LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA JIMBO LA CHEMBA MKOA WA DODOMA 2024 KWA**

### **KUTUMIA MFUMO WA ALAMA ZA VIDOLE (BIOMETRIC VOTERS REGISTRATION\_BVR)**

#### **1.0. Utangulizi**

Jimbo la Chemba ni miongoni mwa Majimbo kumi (10) yaliyopo katika Mkoa wa Dodoma ambayo yalishiriki katika uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura 2024. Kutokana na Ratiba iliyotolewa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Halmashauri iliendesha zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga kura kwa kutumia Mfumo wa alama za vidole yaani Biometric Voters Registration (BVR) katika awamu ya saba kitaifa na awamu ya pili kimkoa iliyojumuisha majimbo ya Chemba, Kondoa mjini na Kondoa Vijijini. Zoezi katika Jimbo la Chemba lilianza Tarehe 11/12/2024 na kumalizika Tarehe 17/12/2024. Zoezi hili limefanyika kwa vituo vyote 315 kwa kuhusisha waendesha vifaa vya bayometriki (BVR Kit operators) 315 na waandikishaji wasaidizi 315.

#### **2.0. Mapokezi ya Vifaa kwa ajili ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura**

Jimbo la Chemba lilipokea jumla ya BVR kit na printer zake 127 kwa ajili ya Mafunzo na BVR Kits zikiwa na printer zake 378 kwa ajili ya uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura ikiwa na mchanganuo wa BVR na printer 315 za kazi na 63 za ziada (Buffer). Pia vifaa mbalimbali vya uboreshaji wa Daftari kama vile Fomu Na. 1,2, 3A, 3B, 4,5A,5B, 6 na 7, PVC Kadi, Ribbon, fulana, Kofia, mabango mbalimbali ya maelekezo, na vitabu vya maelekezo vilipokelewa.

5!

#### **3.0. Semina kwa Maafisa Waandikishaji Wasaidizi ngazi ya Kata, Waandishi na BVR Kit Operators**

Tarehe 04-05/12/2024 ilifanyika semina kwa ajili ya Maafisa Waandikishaji Wasaidizi ngazi ya kata (ARO- kata). Baada ya Maafisa Waandikishaji Wasaidizi ngazi ya Kata kupewa mafunzo juu ya mfumo wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu kwa kutumia Biometric Voters Registration (BVR), Tarehe 08-09/12/2024 Maafisa Waandikishaji Wasaidizi ngazi ya Jimbo wakishirikiana na maafisa Waandikishaji Wasaidizi ngazi ya Kata pamoja na maafisa kutoka tume huru ya taifa ya Uchaguzi walitoa mafunzo kwa BVR operators, Waandishi wasaidizi na waandishi wasaidizi wa akiba waliokuwa wameteuliwa na Halmashauri ya Wilaya baada ya kukidhi vigezo hasa vya ujuzi wa kutumia kompyuta.

#### 4.0 Kuanza kwa zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kutumia mfumo wa BVR

Zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika Jimbo la Chemba lilianza Tarehe 11/12/2024 na kumalizika tarehe 17/12/2024. Tathmini inaonesha kuwa tulifanikiwa kuandikisha wapigakura wapya 37,510 sawa na asilimia 95% ya lengo la kuandikisha wapigakura wapya 39,460. Wapigakura 15463 waliboresha taarifa zao na wapigakura 53 walifutwa kwenye daftari kutokana na sababu mbalimbali.

Kwa Takwimu hizi ni dhahiri kuwa Halmashauri imefanya vizuri kwenye uandikishaji na uboreshaji wa taarifa za wapiga kura kwa asilimia 95% pamoja na changamoto kadhaa zilizojitokeza wakati wa zoezi hilo.

Jedwali lifuatalo linaonesha mchanganuo wa Uandikishaji wa wanachama wapya kwa kila kata.

<b>JIMBO LA CHEMBA TATHMINI YA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA 2024</b>				
<b>S/N</b>	<b>KATA</b>	<b>MALENGO</b>	<b>WALIOJIANDIKISHA</b>	<b>ASILIMIA</b>
1	TUMBAKOSE	585	1,072	183
2	GWANDI	852	1,259	148
3	KIDOKA	1,905	2,688	141
4	OVADA	967	1,290	133
5	LALTA	672	785	117
6	MAKORONGO	1,005	1,163	116
7	KWAMTORO	2,053	2,337	114
8	BABAYU	1,319	1,356	103
9	PARANGA	2,048	2,035	99
10	CHEMBA	1,131	1,119	99
11	MSAADA	851	822	97
12	KIMAHA	1,562	1,431	92
13	GOIMA	1,743	1,590	91
14	SANZAWA	1,857	1,684	91
15	MRIJO	3,230	2,870	89
16	DALAI	2,116	1,838	87
17	FARKWA	1,816	1,574	87
18	SOYA	1,496	1,266	51 85
19	SONGOLO	1,521	1,224	80
20	CHANDAMA	1,222	979	80
21	MPENDO	1,379	1,097	80
22	KINYAMSINDO	814	640	79
23	LAHODA	2,394	1,818	76
24	JANGALO	2,525	1,861	74
25	CHURUKU	1,120	821	73
26	MONDO	1,278	874	68
<b>JUMLA</b>		<b>39,460</b>	<b>37,493</b>	<b>95</b>

#### 4.0. Mafanikio

Kwa ujumla zoezi hili la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika Jimbo la Chemba limefanyika kwa hali ya amani na utulivu kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na maelekezo ya uandikishaji. Pia wadau wa uandikishaji kama vile vyama vya siasa walishirikishwa kikamilifu hatimaye kufanikisha zoezi la uandikishaji kwa asilimia 95. Aidha zoezi hili lilifanyika kwa weledi kwa ushirikiano mkubwa wa Waandishi, BVR Kit Operators, Mafundi toka Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Maafisa Waandikishaji Wasaidizi ngazi ya Kata na Jimbo. Kazi hiyo ilifanyika kwa moyo wa kizalendo na kwa kujituma.

## **5.0. Changamoto**

Changamoto zifuatazo zilijitokeza wakati wa zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura:

- Wananchi kuchanganya zoezi la uandikishaji chini ya TAMISEMI na uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura, na ilichukua siku kadhaa kujua tofauti ya mazoezi haya na ililazimu kufanya matangazo kwa nguvu sana ndipo wananchi wakaelewa.
- Umbali wa maeneo ya Kiutawala wakati wa usimamizi wa zoezi.
- Changamoto ya mvua ambayo ilipelekea BVR 4 kuchelewa kufika kwenye vituo kutokana na mito kujaa na hivyo kupelekea vituo kufunguliwa saa nne asubuhi siku ya kwanza ya uandikishaji.
- Mawakala wa vyama vya siasa kuchelewa kuapa na hivyo kulazimu kufanya kazi bila mawakala.

## **Hitimisho**

Tunapenda kutoa pongezi na shukrani zetu za dhati kwa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, kamati ya ulinzi na usalama ya Wilaya, taasisi za elimu kwa mpigakura pamoja na wadau wa vyama mbalimbali vya siasa kwa ushirikiano waliouonyesha kwa Halmashauri yetu katika kipindi chote cha zoezi hili muhimu la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwani pale ambapo msaada wa hali na mali ulihitajika tuliupata ushirikiano wa kutosha na kwa wakati. Pia napenda kutoa shukrani kwa wataalam toka Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, BVR operators na Waandishi wasaidizi walioshiriki kikamilifu katika zoezi hili kwa moyo wa kizalendo waliouonyesha na hatimaye kufanikisha kazi hii muhimu. Mwisho natoa shukrani za dhati kwa wadau mbalimbali waliofanikisha zoezi hili kama vile vyama vya Siasa, viongozi wa Wilaya na Mkoa licha ya changamoto kadhaa zilizojitokeza lakini mwamko wa wananchi ulikuwa mkubwa kwa karibu vituo vyote vya uandikishaji na zoezi zima kwa ujumla lilienda vizuri na limeisha salama kwa mafanikio makubwa.



MH.MWENYEKITI,  
KAMATI YA FEDHA UONGOZI NA MIPANGO (FUM),  
**CHEMBA.**

## **TAARIFA YA UTEKELEZAJI SHUGHULI ZA TASAF OKTOBA HADI DISEMBA 2024**

### **1.0 Utangulizi**

Mh.Mwenyekiti, ifuatayo ni taarifa ya utekelezaji wa shughuli za TASAF robo ya pili (Oktoba hadi Disemba, 2024. Taarifa hii inaelezea utekelezaji wa shughuli za TASAF kwa robo hii ambayo ni malipo ya Walengwa.

### **2.0 Malipo kwa kaya za TASAF**

Mh.Mwenyekiti, malipo kwa walengwa yalifanyika mara mbili (mwezi Oktoba na Disemba 2024) ambayo ni ya kipindi cha Julai/Agosti na Septemba/Oktoba, 2024.

#### **2.1 Mchangano wa fedha zilizopokelewa**

Halmashauri ilipokea jumla fedha taslimu Sh. **233,101,300** kwa ajili ya shughuli ya malipo ya Walengwa. Kati ya hizo fedha za kulipa Walengwa ni Sh.163,234,000. Hali kadhalika Sh.69,867,300 ni kwa ajili ya uendeshaji na ufuatiliaji wa shughuli katika ununuzi wa dizeli, shajala, matengenezo ya vifaa/gari, malipo ya watekelezaji kama vile wasimamizi, wawezeshaji, madereva, watendaji wa vijiji, wenyeviti wa vijiji, wajumbe wa serikali za vijiji, wajumbe wa Kamati za usimamizi za vijiji (CMC) na polisi.

#### **2.2 Malipo kwa walengwa**

Malipo ya Walengwa wa TASAF yamefanyika kwa njia mbili ambazo ni njia ya taslimu na njia ya mtandao kama inavyobainishwa hapo chini.

##### **2.2.1 Malipo kwa njia ya fedha taslimu**

Mhe.Mwenyekiti, katika kipindi vyote viwili vya malipo (Julai/Agosti na Septemba/Oktoba, 2024) ilitarajiwa kulipa jumla ya kaya 3,085 kwa fedha idhinishwa kiasi cha Sh.163,234,000. Fedha zilizolipwa ni Sh.162,862,000 na zilibaki Sh.372,000 na zilizorudishwa TASAF Makao Makuu (Kiambatisho).

##### **2.2.2 Malipo kwa njia ya mtandao**

Mhe.Mwenyekiti katika vipindi hivi vya malipo jumla ya fedha iliyolipwa kwa walengwa kwa njia ya mtandao ni **93,418,000/=** kwa kaya 1916.

### 3.0 Changamoto

Pamoja na mafanikio ya utekelezaji wa shughuli, kuna baadhi ya changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji kama inavyooneshwa kwenye jedwali lifuatalo;

Jedwali Na.1: Changamoto

<b>Changamoto</b>	<b>Sababu</b>	<b>Utatuzi/Mikakati</b>
Baadhi ya Walengwa wanaopokea fedha kwa njia ya simu kutopokea malipo	Kufungiwa huduma ya kupokea fedha	1.Kufanya marekebisho ya namba zao za simu 2.Kuwarudisha kwenye malipo ya taslimu

### 4.0 Matarajio

Kuendelea kulipa ruzuku kwa kaya zilizobaki kwenye Mpango

Mh.Mwenyekiti naomba kuwasilisha

Simon Z. Butondo  
Kny: Mkurugenzi Mtendaji (H/W)  
**CHEMBA.**

Kiambatioho: Muhtasari wa malipo ya kaya za TASAF Julai - Agosti na Septemba-Oktoba 2024															
Na	Kijiji	Julai - Agosti 2024					Septemba - Oktoba 2024								
		Kaya tarajawa	Zilizolipwa	Zisizolipwa	Sababu	Fedha idhinishwa	Fedha iliyolipwa	Fedha baki	Kaya tarajawa	Zilizolipwa	Zisizolipwa	Sababu	Fedha idhinishwa	Fedha iliyolipwa	Fedha baki
1	Babayu	12	12	0		390,000	390,000		12	12	0		382,000	382,000	
2	Chase	16	16	0		506,000	506,000		25	25	0		752,000	752,000	
3	Chinyika	21	21	0		606,000	606,000		32	32	0		938,000	938,000	
4	Masimba	25	25	0		752,000	752,000		33	33	0		1,042,000	1,042,000	
5	Mpendo	9	9	0		246,000	246,000		11	11	0		310,000	310,000	
6	Chandama	17	17	0		496,000	496,000		24	24	0		710,000	710,000	
7	Mapango	60	60	0		1,956,000	1,956,000		64	64	0		2,114,000	2,114,000	
8	Chambalo	31	31	0		988,000	988,000		25	25	0		764,000	764,000	
9	Chemba	35	35	0		1,042,000	1,042,000		32	32	0		1,018,000	1,018,000	
10	Kambi ya Nyasa	44	44	0		1,338,000	1,338,000		57	57	0		1,744,000	1,744,000	
11	Churuku	11	11	0		300,000	300,000		20	20	0		662,000	662,000	
12	Jinjo	13	13	0		392,000	392,000		24	24	0		776,000	776,000	
13	Kinkima	14	14	0		478,000	478,000		29	29	0		872,000	872,000	
14	Tandala	3	3	0		78,000	78,000		3	3	0		78,000	78,000	
15	Itirikwi	8	8	0		258,000	258,000		8	8	0		266,000	266,000	
16	Dalai	13	13	0		454,000	454,000		14	14	0		484,000	484,000	
17	Mtakuja	19	19	0		726,000	726,000		19	19	0		726,000	726,000	
18	K/Maziwani	20	20	0		578,000	578,000		24	24	0		696,000	696,000	
19	Piho	23	23	0		720,000	720,000		27	27	0		822,000	822,000	
20	Njoni Muone	30	30	0		890,000	890,000		34	34	0		1,072,000	1,072,000	
21	Donsee	0	0	0					0	0	0				
